Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU NA MUUNGANO WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 039/2020**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 13 Juni 2023**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) ilitoa hukumu katika kesi ya *Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

*Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania* (Waleta Maombi) ni Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) yaliyosajiliwa na kufanya kazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yakiwa na hadhi ya mwangalizi kupitia Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Tume). Waleta Maombi walidai kuwa kwa kutunga kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) ambacho kinaelezea makosa yaisyokuwa na dhamana, Mjibu Maombi alikiuka Kifungu cha 1, 2, 6 na 7 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba).

Mahakama, kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki), iliona kwamba ilipaswa, kwanza, kuamua endapo ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi. Katika suala hili, Mjibu Maombi aliweka pingamizi kuhusu mamlaka yake binafsi akisema kuwa Waleta Maombi hawajathibitisha kwamba walifurahia hadhi ya kuwa waangalizi mbele ya Tume. Katika suala hili, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi waliwasilisha barua kutoka Tume inayoonyesha kwamba Kituo cha Kisheria na Haki za Binadamu kilikuwa na hadhi ya mwangalizi mbele ya Tume. Aidha, Mahakama iliona kuwa Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania waliorodheshwa kwenye tovuti ya Tume kuwa ni Shirika Lisilo la Kiserikali wakiwa na hadhi ya mwangalizi mbele ya Tume. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka binafsi ya kuchunguza kesi hiyo.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Mjibu Maombi, hata hivyo, Mahakama ilivichunguza. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kisheria kwa kuwa Maombi yalionesha madiai ya ukiukaji wa haki zinazolindwa chini ya Mkataba. Mahakama pia iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Mkataba, Itifaki na alikuwa ameweka Azimio lililohitajika chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki. Mwisho, pia iligundua kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi. Kwa hivyo Mahakama ilihitimisha kwamba ilikuwa na mamlaka ya kisheria kusilikiliza Maombi.

Chini ya Kifungu cha 6 cha Itifaki, Mahakama ina wajibu wa kuamua endapo matakwa ya ukubalifu, kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 56 cha Mkataba na Kanuni ya 50 ya Kanuni za Mahakama (Kanuni), yametimizwa. Katika suala hili, Mahakama kwanza ilizingatia mapingamizi yaliyotolewa na Mjibu Maombi kuhusu kutokamilisha taratibu za ndani, Maombi yakiwa hayajawasilishwa kwa wakati unaofaa, jambo hilo kuwa lilikuwa limeshatatuliwa tayari na kutofautiana kwa Maombi na Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika au Mkataba.

Kuhusiana na kukamilisha taratibu za ndani, Mahakam ilibaini kwamba kanuni hiyo kimsingi hahihitaji kwamba kisi inayowasilishwa mbele ya Mahakama lazima pia iwasilishwe mbele ya mahakama za ndani na Mleta Maombi yuleyule hasa kwa kesi zenye maslahi ya umma. Mahakama ilibaini tena baadhi ya watu binafsi walikuwa tayari wanahoji uhalali wa kikatiba wa kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai katika mahakama za kitaifa na mfano wa mwisho ukiwa, kesi ya *Dickson Sanga Paul* iliyoamuliwa tarehe 5 Agosti 2020 na Mahakama ya Rufaa ikiamua kuwa kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kilikuwa cha kikatiba. Katika suala hili, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi wasingeweza kutarajiwa kufanikiwa kwenye mahakama za kitaifa kuhusu kesi yenye maslahi ya umma kuhusiana na suala lilelile ambalo tayari limeamuliwa na Mahakama ya Rufaa, kwa kuwa kusingekuwa na uwezekano wa mafanikio, kwa hivyo kufanya njia hiyo isiwe na ufanisi. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Maombi yalizingatia Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusiana na endapo Maombi yaliwasilishwa ndani ya wakati unaofaa baada ya kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama ilibainisha kuwa kesi ya Mahakama ya Rufaa kwenye kesi ya *Dickson Sanga Paul* iliamuliwa mnamo tarehe 5 Agosti 2020, ambayo ni miezi mitatu (3) na siku kumi na tano (15) kabla ya Waleta Maombi kufika Mahakamani. Mahakama iliona kuwa kipindi hiki kilikuwa kinafaa na hivyo Maombi yalizingatia Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusu endapo suala hilo lilikuwa limeshatatuliwa tayari kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(g) ya Kanuni hizo, Mahakama iliona kuwa hoja ya Mjibu Maombi ilikuwa ni kwamba uamuzi wa Mahakama katika kesi ya *Anaclet Paulo dhidi ya Tanzania* (kesi ya Paulo) ilisuluhisha masuala yaliyoibuliwa katika kesi ya sasa na kwa hivyo Maombi yanapaswa kutangazwa kuwa hayafai kuwasilishwa. Ili kuamua endapo masuala yaliyo katika kesi ya sasa yametatuliwa, kwa kuzingatia busara yake ya kisheria, Mahakama ilipima kwa kuangalia masuala matatu muhimu ya manufaa, kulingana na hali ilikuwa ikiongezeka. Jambo la kwanza ni kuhusu utambulisho wa wahusika. Katika suala hili, Mahakama ilibainisha kuwa Mjibu Maombi katika kesi ya *Paulo* na kesi ya sasa ni yuleyule, yaani, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, Waleta Maombi walikuwa tofauti katika kesi ya *Paulo* , Mleta Maombi alikuwa mtu binafsi wakati katika kesi ya sasa, Waleta Maombi ni mashirika mawili yasiyo ya kiserikali. Hivyo Mahakama ilibaini kuwa hitaji la utambulisho wa wahusika halijatimizwa. Hata hivyo, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi hawapaswi kuwa wale wale kila wakati, ilimradi wanatafuta kupata maslahi yanayofanana. Katika suala hili, Mahakama ilibainisha kuwa Waleta Maombi katika kesi ya sasa walikuwa wakifuatilia maslahi tofauti ukilingania na yale katika kesi ya *Paulo* . Katika suala hili, Mahakama ilibainisha kuwa Mleta Maombi katika kesi ya *Paulo* , alitaka kulinda haki za mtu binafsi zinazodaiwa kukiukwa katika kesi yake na kuhusiana na kesi hiyo mbele ya mahakama za kitaifa. Kwa upande mwingine, Waleta Maombi katika kesi ya sasa ni mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotafuta kulinda haki za umma kwa ujumla, kutokana na kesi ya maslahi ya umma mbele ya mahakama za kitaifa.

Zaidi ya hayo, Mahakama ilibainisha kuwa maombi ya Maombi ya Mleta Maombi katika kesi ya *Paulo* na maombi ya Waleta Maombi katika kesi ya sasa yalikuwa tofauti. Katika suala hili, Mahakama alibainisha kuwa Bw. Paulo aliomba Mahakama, kutokana na ukiukaji unaodaiwa, impe msaada wa kisheria na kumpa fidia na usaidizi mwingine ambao Mahakama itaona unafaa. Kinyume chake, Waleta Maombi katika kesi ya sasa, waliiomba Mahakama kuamuru Mjibu Maombi kuchukua hatua za kikatiba na za kisheria ili kuhakikisha haki chini ya Mkataba; iamuru kwamba watuhumiwa wote na watuhumiwa wanaoshtakiwa kwa kosa lisilodhaminika waachiliwe kwa dhamana ndani ya mwezi mmoja, kulingana na mazingira ya kila kesi. Kwa hivyo, Mahakama iliona kuwa Mleta Maombi katika kesi ya Paulo alitafuta njia binafsi lakini katika kesi ya sasa, Waleta Maombi walitafuta njia ya kikatiba na kisheria kwa maslaji ya umma.

Hatimaye, Mahakama iliona kwamba haikupokea hoja zozote katika kesi ya *Paulo* kuhusu Sehemu ya 148(5) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai zaidi ya haki ya uhuru kuhusu athari za Sehemu ya 148(5) (a) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai wala haikuzingatia hoja kuhusu kuondolewa kwa uamuzi wa kimahakama ya Mahakama na haki ya kusikilizwa kutokana na utekelezaji wa Sehemu ya 148(5) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kama ilivyoonyeshwa na Waleta Maombi kwenye kesi

ya sasa. Kwa hivyo, Mahakama ilibaini utambulisho wa madai kuwa yapo chini ya mipaka ya Sehemu ya 148(5)(a) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Vivyo hivyo, Mahakama ilibaini kwamba uamuzi wa kwanza kuhusu uzingatiaji wa sheria ambao ni kiungo cha mwisho cha "usuluhishi" ulizingatiwa tu kuhusiana na Sehemu ya 148(5)(a) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Kwa hivyo, Mahakama ilihitimisha kuwa ni mazingatio tu ya Sehemu ya 148(5)(a) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ndiyo ilikuwa imekamilika na hivyo Mahakama haikuzuiliwa kuamua endapo Sehemu ya 148(5) (b)-(e) ya Sheria wa Mwenendo wa Makosa ya Jinai na kwa kiasi hiki, Waleta Maombi walikidhi matakwa yaliyo chini ya Kanuni ya 50(2) (g) ya Kanuni za Mahakama.

Mahakama ilikataa pingamizi hilo kutokana na kutofuata Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika au Mkataba, wakiona kuwa Waleta Maombi walitaka kulinda haki zilizohakikishwa chini ya Mkataba baada ya madai ya kukiuka Vifungu vya 1, 2, 6 na 7 vya Mkataba. Kwa hivyo, walikuwa wamezingatia Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni hizo.

Ingawa masharti mengine ya ukubalifu hayakupingwa na Mjibu Maombi, Mahakama ililazimishwa na Kifungu cha 6 cha Itifaki kuhakikisha kuwa yametimizwa. Katika suala hili, iliona kwamba, Waleta Maombi walikuwa wametambuliwa kwa jina kwa kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Aidha, Mahakama ilibaini kuwa lugha iliyotumiwa katika Maombi haikuwa ya kudharau au kumtukana Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama na kwamba Maombi hayakuzingatia tu habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama. Kwa hivyo, Mahakama ilitangaza kwamba Maombi yanakubalika kwa kiwango cha madai kuhusu Vifungu vidogo vya 148(5)(b)-(e) vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria wa kesi hiyo, Mahakama ilizingatia endapo Vifungu vidogo vya 148(5)(b) na (e) vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kilikuwa cha kibaguzi na hivyo kukiuka Kifungu cha 2 cha Mkataba. Mahakama ilibaini kwamba Vifungu vidogo vya 148(5)(b) na (e) vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinaikataza mahakama kuzingatia maombi ya dhamana ya watuhumiwa ambao wametumikia kifungo kisichozidi miaka mitatu na wale ambao wameshtakiwa kwa makosa yanayohusiana na mali yenye thamani ya zaidi ya Shilingi za Kitanzania milioni kumi (TZS 10,000,000). Mahakama iliona kuwa, kwa kweli, vifungu vidogo vilivyotajwa hapo juu vinawatendea vibaya watuhumiwa hao ukilinganisha na watu walioshtakiwa kwa makosa mengineyo yanayoangukia nje ya Sehemu ya 148(5) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Vifungu vidogo vya 148(5)(b) na (e) vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vilikuwa vya kibaguzi na hivyo kukiuka Kifungu cha 2 cha Mkataba.

Kisha Mahakama ilizingatia endapo Vifungu vidogo vya 148(5)(b) na (c) vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vilikiuka haki ya kudhaniwa kuwa hawana hatia. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa Mahakama kuzuiwa kuzingatia maombi ya dhamana yaliyotolewa chini ya Kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai si muhimu wala kuwa sambamba na lengo ambalo inataka kufikia na hivyo ilikiuka haki ya kudhaniwa kutokuwa na hatia chini ya Kifungu cha 7(1)(b) cha Mkataba.

Aidha, Mahakama iliamua iwapo Vifungu vidogo vya 148(5)(b) na (c) vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vilikiuka haki ya kusikilizwa. Mahakama ilibaini kuwa Sehemu ya 148(5) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai haimpi afisa wa mahakama chaguo lolote la kutoa dhamana pale ambapo mtuhumiwa ataangukia chini ya moja ya makundi yaliyoorodheshwa chini ya Sehemu ya 148(5) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Iliona kwamba, hii inamnyima mtuhumiwa haki yake ya kusikilizwa na hasa, kuwasilisha hali yake ya kipekee ambayo inaweza kumruhusu afisa wa mahakama kutoa dhamana. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Vifungu vidogo vya 148(5)(b) na (c) vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vilikiuka haki ya kusikilizwa.

Mahakama ilibaini tena kwamba, kama matokeo ya kupata ukiukaji mwingine wa Mkataba katika kesi ya sasa, Kifungu cha 1 cha Mkataba kilikiukwa pia.

Kwa upande wa fidia, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi kuchukua hatua zote muhimu za kikatiba na kisheria, ndani ya muda unaofaa usiozidi miaka miwili (2), ili kuhakikisha vifungu vidogo vya 148(5) (b) - (e) vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinarekebishwa na kuendana na masharti ya Mkataba ili kuondoa ukiukwaji wowote wa Mkataba na vyombo vingine vilivyoidhinishwa na Mjibu Maombi. Hata hivyo, Mahakama ilikataa ombi la kuamuru Mleta Maombi kuwaachia huru watu wote wanaoshtakiwa kwa makosa yasiyokuwa na dhamana ndani ya mwezi mmoja (1) tangu tarehe ya hukumu hii, ikibainisha kuwa suala la endapo dhamana inapaswa kutolewa au kukataliwa linapaswa kuachwa kwenye mahakama za ndani kuamua endapo watahitaji kuzingatia hali ya mtu binafsi katika kila kesi.

Mahakama kwa hiari yake iliamuru Mjibu Maombi achapishe Hukumu ndani ya kipindi cha miezi mitatu (3) tangu tarehe ya kupokea taarifa, kwenye tovuti za Mahakama na Wizara ya Katiba na Sheria, na kuhakikisha kuwa hati ya Hukumu inaendelea kupatikana kwa angalau mwaka mmoja (1) baada ya tarehe ya kuchapishwa.

Mwisho, Mjibu Maombi aliamriwa kutoa taarifa kuhusu hatua zilizochukuliwa kutekeleza hukumu hii ndani ya miezi kumi na miwili (12) baada ya kupokea taarifa ya hukumu.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake mwenyewe.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti kwenye: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0392020

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*

.